

AHSANTE MAMA




USIONDOKE, SUBIRI CHAKULA, MAMA WATOTO AMERUDI



MAMA TUNU, JIRANI ANAAGA

JIRANI USIONDOKE, NAMALIZA KUNAWA NIWAADALIE CHAKULA



NAJIVUNIA MKE WANGU ANAJUA MAPISHI, MKEKA NA KIKAPU HICHO JUU KASUKA PIA



JIRANI SUBIRI NIKUNAWISHE KWANZA

SHEMEJI MBONA NILINAWA KABLA SIJAJA HAPA?



JIRANI, MAJI PEKEE HAYAWEZI KUIWA WADUDU WANAOAMBUKIZA MAGONJWA YA KUHARA

TENA JIRANI AMENISIMULIA, FAMILIA YAKE INASUMBULIWA NA MAGONJWA YA MARA KWA MARA



NI MUHIMU SANA KUNAWA KWA SABUNI KABLA YA KULA NA BAADA YA KUTOKA CHOOINI

LAKINI KUNAWA KWA SABUNI MIMI HUWA NAONA USUMBUFU



NIMEMTAWAZA MTOTO, ACHA NINAWE NIJE NIWAONYESHE NJIA RAHISI YA KUNAWA MIKONO



UNAHTAJI DUMU TUPU KAMA HILI..



..KISHA ULITOBEO TUNDU UBAVUNI..



..HALAFU PITISHA KAMBA JUU..




..NING'INIZA KWENYE MTI AU MITI MAALUMU YA KUNING'INIZIA KIBUYU CHIRIZI



..FUNGA KAMBA KWENYE MDOMO WA KIBUYU CHIRIZI KISHA IFUNGE KWENYE KIJITI CHA KUKANYAGIA..



..TOBOA TUNDU KATIKATI YA SABUNI NA KISHA PITISHA KAMBA



..UNAWEZA KUKATA CHUPA YA PLASTIKI NA KUFUNIKA SABUNI DHIDI YA YUMBI NA MVUA



JIRANI AHSANTE KWA ELIMU, NAKWENDA KUTENGENEZA KIBUYU KWA AJILI YA FAMILIA YANGU

